AJIS

ACTION FOR JUSTICE IN SOCIETY



# MIRATHI NA WOSIA

## UTANGULIZI WA SHIRIKA.

AJISO ni Shirika lisilo la Kiserikali ambalo lilianzishwa na kikundi cha Wanawake wapatao kumi na tano (15) katika mkoa wa Kilimanjaro mnamo mwaka 1998. Lilisajiliwa kama shirika lisilo la Kiserikali ambalo si la Kidini, Kisiasa, wala kibaishara kwa nia a kugawana faida.

Kimsingi, Shirika lilianzishwa kwa madhumuni ya kuwainua na kuwawezesha Wanachama wake na Wanawake kwa ujumla kupata habari juu ya haki za binadamu, sheria pamoja na kukuza uchumi wao.

## MAONO.

AJISO inatamani jamii ambayo inathamini na kuheshimu haki na usawa wa jinsia.

## MIKAKATI YA SHIRIKA.

- Kutoa ,saada wa kisheria na kukuza uelewa juu ya Haki za Binadamu kwa Wanawake, Watoto na Makundi yaliyo pembezoni.
- Kuhamasisha uwezeshaji kiuchumi, ili kupata huduma bora za jamii na kuboresha maisha na uchumi wa wanawake wanaoishi maeneo ya pembezoni.
- Kuchapisha makala na vijarida mbalimbali kuhusu elimu ya sheria jamii na haki za binadamu kwa lengo la kujenga uwezo kwa jamii kuhusu sheria zonazowalinda na wajibu wao.
- Kuhamasisha ushiriki wa wanawake na makundi yaliyoko pembezoni kushiriki kikamilifu katika vyombo vya maamuzi kwenye jamii mfano, katika ngazi ya family, serikali za mtaa/vijiji, kata, n.k.
- Kuimarisha uwezo wa shirika kwa kutunisha mfuko na kujenga uwezo kwa watendaji, kwa ajili ya maendeleo endelevu.
- Kukuza mahusiano mazuri ya kikazi na vyombo vya habari, taasisi za tafiti mbalimbali na mashirika yenye malengo sawa na AJISO.

## 1.0 WOSIA.

**Je unafahamu wosia na umuhimu wake ?**

Wosia ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake AU tamko ambalo linaweza kuwa la Mdomo au la Maandishi, linalofanywa na mtu yeyote likionyesha jinsi anayotaka mali yake igawanywe, au isimamiwe baada ya kifo chake, namna mazishi yake yatakavyokuwa, mfano mahali atakapozikwa n.k.

**Kuna Aina Mbili za Wosia.**

i) Wosia wa Mdomo,

ii) Wosia wa Maandishi**.**

Wosia wa Mdomo, hutolewa kwa mdomo na unapaswa kushuhudiwa na watu wasiopungua wanne, wawili kati yao lazima wawe wanaukoo wa Muwosia. Katika wosia huu kama mashahidi watakufa kabla ya muusia kufa, basi wosia hautakubalika. Mwenyewe kama anataka kuusia mali zake, atoe wosia mpya.

Wosia wa Maandishi, hutolewa na Muwosia anayejua kusoma na kuandika, na unatakiwa uandikwe kwa kalamu ya wino usiyofutika au upigwe chapa. Wosia huu lazima ushuhudiwe na watu wasiopungua wawili wanaojua kusoma na kuandika.

**ANGALIZO.**
*Muwosia asiyejua kusoma na kuandika anaweza kutoa Wosia wake kwa maandishi na kutia saini ya kidole gumba cha mkono wa kulia. Wosia huu hushuhudiwa na watu wanaojua kusoma na kuandika na mmoja wao lazima awe mwanandugu.*

**SIFA ZA MUWOSIA.**

- Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 18;
- Awe na akili timamu;
- Afanye kwa hiari yake na bila kulazimishwa.

Kama Muwosia ni mgonjwa wakati wa kuandika Wosia, basi Daktari ni lazima ahusishwe.

Wosia unaweza kuhifadhiwa sehemu yeyote yenye usalama, ili kuepuka uwezekano wa kufanyiwa mabadiliko na mtu asiye Muwosia. Inashauriwa sehemu kama vile, Benki, Mahakamani, Kanisani, n.k.

## 2.0 MIRATHI.

Ni taratibu mbalimbali za kisheri **zinazoongoza**uangalizi, usimamizi, umuliki na hatimaye ugawaji wa mali nap engine hata kumaliza madeni ya marehemu pamoja na mazishi.

### 2.1 Aina za Mirathi.

Kuna aina kuu mbili za mirathi.

a) Mirathi palipo na Wosia. Hii hutokea wakati ambapo marehemu kabla ya kufa aliacha maandishi / matamshi au maelezo ya namna mali yake itakavyoshughulikiwa itakavomilikiwa baada ya kifo chake.

b) Mirathi pasipo wosia. Hii hutokea pale ambapo marehemu hakuacha wosia, ambapo warithi halali wa marehemu hulazimika kuchagua kupitia mahakama / msimamizi au wasimamizi wa mirathi hiyo.

## 3.0 TARATIBU ZA KISHERIA KATIKA MIRATHI.

a) **Panapokuwa na wosia.**

i) Ndani ya siku 30 baada ya kifo cha marehemu wahusika wanapaswa kusajili kifo cha marehemu kwenye ofisi ya vizazi na vifo ambayo iko kwa mkuu wa wilaya wa kila wilaya. Kama wahusika watachelewa kuandikisha kifo hicho ndani ya siku 30 wafike kwenye ofisi hiyo ya vizazi na vifo kwa maelezo. Kifo kinasajiliwa kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya yeyote. Kama kuna matatizo kuhusu wapo kifo kisajiliwe, whusika wanaweza kuwasiliana na msajili mkuu wa Vizazi na vifo Makao Makuu Dar es Salaam.

ii) Mara baada ya usajili wa kifo cha marehemu, waombaji wanaweza kufungua shauri la mirathi mahakamani, wakiambatanisha nakala ya wosia ulioachwa na marehemu na cheti cha kifo cha marehemu.

iii) Baada ya kuwasilisha maombi ya mirathi, mahakama kwa kawaida huroa tangazo la mirathi kwa muda wa siku 90 kwenye gazeti linalosomwa na watu wengi au katika mbao za mahakama. Lengo ni kuwawezesha wale wasioridhika na usimamizi huo kupeleka pingamizi mahakamani. Mahakama inauwezo wa kufupisha kipindi hiki cha tangazo la siku 90 kwa kutoa tangazo la muda mfupi zaidi.

iv) Baada ya siku 90 kuisha au muda mfupi zaidi uliowekwa na mahakama bila pingamizi kutolewa, mahakama itamthibitisha muombaji kuwa mrithi au mtekelezaji wa wosia wa marehemu.

v) Endapo muombaji ni mtekelezaji tu wa wosia wa marehemu atalazimika kutekeleza, kuendeleza taratibu za kugawa mali za marehemu kama ifuatavyo;

- Kukusanya mali na madeni ya marehemu na pia kutambua anaowadai.
- Kutayarisha taarifa ya awalai ya maelezo/ufafanuzi wa mali zote na madeni ya marehemu (inventory).
- Msimamizi / mtekelezaji wa wosia atagawa mali kwa mujibu wa wosia.
- Kutoa taarifa ndani ya miezi sita ya ukamilishwaji wa zoezi hilo limeendeshwa sawa.

- ➢ Mahakama kufunga jalada la mirathi kama zoezi la ugawaji limeendeshwa sawa na kukamilika.

b) **Pasipo na Wosia.**

i) Utaratibu wa usajili wa kifo ni kama ilivyo kwenye utaratibu wa mirathi palipo na wosia.

ii) Msimamizi au Wasimamizi wa mirathi huteuliwa au kuchaguliwa na kikao cha wana ndugu au ukoo.

iii) Mbali na cheti cha kifo cha marehemu, maombi ya usimamizi wa mirathi yanatakiwa kuambatanishwa na nakala ya kikao cha wanandugu cha kumchagua msimamizi wa mirathi.

iv) Taratibu la tangazo la siku 90 au muda mfupi pungufu (chini ya hapo) ni sawa na zile zinazotumika pale palipo na wosia.

v) Taratibu za ukusanywaji wa mali na madeni ya marehemu pamoja na uandaaji wa taarifa ya awali ya maelezo ya mali za marehemu na maeni, zinafanana na zile zilizoelezwa kwenye mirathi palipo na wosia.

vi) Msimamizi wa Mirathi atagawa mali ya marehemu kwa mujibu wa sheria husika yaani inatumika kwenye mirathi hiyo.

vii) Kutoa au kupeleka taarifa ya ugawaji wa mali za marehemu mahakamani kwa madhumuni ya kufunga jalada (ndani ya kipindi cha miezi 6).

## 4.0 PANAPOKUWA NA PINGAMIZI.

Ndani ya kipindi cha siku 90 au pungufu (chini ya hapo) cha tangazo la mirathi kwenye mahakama yoyote, asiyeridhika na kuthibitishwa kwa mtekelezaji wosia ama kuteuliwa kwa msimamizi wa mirathi, mtu huyo anaweza kupeleka pingamizi lake mahakamani.

Mara baada ya mahakama kusikiliza pingamizi hilo inawezekana kumchukulia mpingaji kama mdaiwa (objector) hata baada ya kuisha kwa muda wa siku 90 au muda pungufu ya hapo uliowekwa na mahakama msimamizi kuteuliwa kama kulikuwa na Kughushi au udanganyifu kuhusiana na usimamizi, basi maombi yanaweza kupelekwa mahakamani kutaka msimamizi aondolewe na usimamizi wake kutenguliwa.

**IKUMBUKWE.**

*Kutopeleka taarifa ya kukamilika kwa usimamizi wa mirathi ni kosa la jinai, hivyo msimamizi wa mirathi ni lazima atomize majukumu yake.*

## 5.0 MGAWANYO WA MALI YA MAREHEMU.

- Pale palipo na wosia mara nyingi mgawanyo wa mali ya marehemu hufanywa kwa kuzingatia wosia. Ugumu hujitokeza pale pasipo na wosia ambapo ugawaji wa mali hutegemea sheria mbalimbali kutengemeana na wahusika.
- Hapa nchini kwetu Tanzania sheria zifuatazo kwa kiwango kikubwa huhusika kwa namna moja au nyingine na mambo ya ugawaji wa mali au urithishwaji wa mali ya marehemu.

i) **Sheria ya urithi ya India ya mwaka 1865;**

Hii inatumika pale ambapo itaonekana kwamba marehemu alikuwa hafuati sheria za kiislamu wala taratibu za kimila.

**Mgawanyo wa mali kwa mujibu wa sheria ya urithi ya India;**

- Kama marehemu ameacha mjane na watoto, atapata 1/3 na watoto 2/3 ya mali yote ya marehemu.
- Na kama marehemu hakuacha watoto, mjane atapata ½ na ½ nyingine hugawanywa sawasawa kati ya wazazi, kaka, na dada za marehemu.

**Zingatia.**

*Kwa mujibu wa sheria hiyo watoto wan je ya ndoa hawana haki ya kurithi isipokuwa tu kama kuna wosia na katika wosia huo wamerithishwa mali.*

ii) **Sheria ya Kiislamu.**

Hii hutumika kwa wafuasi wa dini ya kiislamu.

iii) **Sheria ya Kimila.**

Hii hutumika pale ambapo marehemu aliishi kwa kufuata mila na desturi za kabila lake.

### 5.1: Mgawanyo wa mali ya marehemu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

- Warithi wakuu katika sheria ya kiislamu huwa ni mke au wake, mama, na watoto.
- Watoto wa kiume hustahili kupata mara mbili zaidi ya watoto wa kike.
- Wajane (wake wa marehemu) wasiozidi wanne hupata 1/8 ya mali ya marehemu kama marehemu ameacha watoto. Na kama hakuacha watoto ¼ ya mali ya marehemu.
- Baba na mama hupata 1/6 kama marehemu aliacha watoto.

**Zingatia:**

*Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa hana haki ya kurithi isipokuwa kuna wosia.Pia kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu Muislam haruhusiwi kuwosia mali yake yote, anaweza kuwosia 1/3 tu ya mali yake, na 2/3 ni lazima igawanywe kwa warithi wake halali kufuatana na sheria ya kiislamu.*

**5.2: Mgawanyo wa mali ya marehemu kwa mujibu wa sheria za kimila.**

- Hizi zimo katika kanuni za urithi (tangazo la serikali namba 436, la mwaka 1963).
- Kwa mujibu wa sheria hizi kama marehemu ameacha watoto wa kiiume na wa kike hao ndio warithi pekee wa mali ya baba yao.
- Kama marehemu hakuacha watoto mali yake itarithiwa na baba, mama, kaka, dada, wajomba na shangazi zake. Mtoto wa kiume wa nyumba kubwa hupata sehemu kubwa ya mali akifuatiwa na watoto wengine wa kiume, na mwisho watoto wa kike wa nyumba yeyote ile hupata kiasi kidogo zaidi.
- Kwa mujibu wa sheria hii wajane hawajapewa haki ya kurithi, mjane mwenye watoto sheria inampa haki ya kuishi na kutegemea watoto wake ambao watarithi mali ya marehemu mume wake.

**Zingatia:**

- Watoto wa anje ya ndoa hawaruhusiwi kurith chochote isipokuwa kama walihalalisha kufuatana na mila za kabila husika.
- Mali ya marehemu kwa lengo la mirathi inahusisha mali binafsi za marehemu na si vinginevyo.
- Mjane ambaye hana mtoto/watoto atabaki katika nyumba ya marehemu na kuitumia wakati wa uhai wake, ambapo baada ya kifo chake hugawiwa kwa warithi halali wa marehemu mume wake.

## 6.0 WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI.

1. Ndani ya miezi 6 baada ya kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi anawajibika kutoa orodha na kiasi cha mali alizoacha marehemu, fedha taslimu, madeni pamoja na idadi ya warithi halali wa marehemu anaotegemea kuwagawia mali za marehemu.
2. Kukusanya kwa uaminifu mali za marehemu.
3. Kuorodhesha madeni yaliyoachwa na marehemu pamoja na kuyalipa madeni hayo toka kwenye mali alizoacha marehemu.

4. Kulipa gharama za mazishi na gharama za kuendesha mirathi toka kwenye mali za marehemu.
5. Kugawa mali za marehemu kwa warithi halali kama marehemu atakuwa ameacha wosia, msimamizi wa mirathi atagawa kufuatana na wosia alioandika marehemu na kama hakuna wosia atagawa kulingana na sheria inayotumika kwenye mirathi kama ni sheria ya kiislamu, kimila, au kiserikali (yaani sheria ya mirathi ya india 1865).
6. Kushitaki ambapo marehemu angeshitaki ili kudai haki zake au kujibu mashitaka ya madai pale ambapo kutakuwepo na mdai dhidi ya marehemu (msimamizi wa mirathi).
7. Kusikiliza maelekezo yanayotolewa na mahakama kuhusiana na mirathi anayoendesha.
8. Kutoa taarifa mahakamani inayoeleza alivyoendesha mirathi na kugawa mali kwa warithi wa marehemu na hatimaye mirathi kufungwa.

## 7.0 HITIMISHO.

Ni muhimu kuzingatia kwamba msimamizi wa mirathi ni mtu anayechukua nafasi ya marehemu kisheria, mali zote za marehemu kisheria na mali zote za marehemu zitakuwa chini ya uangalizi wake lakini haziwi zake binafsi.

Msimamizi wa mirathi si mrithi wa mali za marehemu anaweza kurithi pale ambapo yeye licha kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ni mrithi halali wa marehemu kama vile ni mtoto wa marehemu.

Pia warithi wa marehemu wana haki kisheria kufungua shauri la madai dhidi ya msimamizi wa mirathi kama msimamizi wa mirathi atashindwa kutimiza wajibu wake, kufuja au kuiba mali ya marehemu na kuwakosesha haki warithi halali.

AJISO
ACTION FOR JUSTICE IN SOCIETY

Kimetayarishwa na:
**Action for Justice in Society (AJISO)**
S.L.P 272 Moshi, Tanzania
Simu; 0783 660 500
Barua pepe: ajisotz@yahoo.com
www.ajiso.org